SURA YA 19

SHERIA YA KUZUIA UGAIDI, 2002

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Jina*

SEHEMU I

VIFUNGU VYA UTANGULIZI

1. Jina fupi.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA II
KUZUIWA KWA VITENDO VYA KIGAIDI

4. Maana na kuzuiwa kwa vitendo vya kigaidi.
5. Kosa la kushiriki mkutano wa kigaidi.
6. Kosa la kikundi kilichopigwa marufuku kwa ajili ya kitendo cha kigaidi.
7. Kuunga mkono ugaidi.
8. Kumhifadhi gaidi.
9. Umiliki wa vitu, habari n.k visivyo ruhusiwa.
10. Katazo dhidi ya vitisho vya vitendo vya kigaidi vya uongo.
11. Kipaumbele katika kutumika.

SEHEMU YA III
VYOMBO MAALUM

12. Ugaidi wa kimataifa.

SEHEMU YA IV
MAKOSA YA JINAI

13. Kutoa au kukusanya fedha ili kutenda vitendo vya kigaidi.
14. Kukusanya mali au kutoa mali na huduma kwa ajili ya vitendo vya kigaidi.
15. Kutumia mali kwa ajili ya kutenda vitendo vya kigaidi.
16. Mpango wa kuhifadhi/kuweka au kulinda mali ya kigaidi.
17. Kushughulika na mali inayomilikuwa au kuangaliwa na vikundi vya kigaidi.
18. Kutafuta na kutoa msaada kwa vikundi vya kigaidi kwa ajili ya kutenda ugaidi.
19. Kuhifadhi watu wanaofanya kitendo cha ugaidi.
20. Kutoa silaha kwa kikundi cha kigaidi.
21. Kuajiri watu kuwa wajumbe wa vikundi vya kigaidi au kushiriki katika kitendo cha kigaidi.

22. Kuhamasisha au kusaidia kutendeka kwa vitendo vya kigaidi katika nchi za nje.
23. Kuhamasisha makosa ya jinai.
24. Kula njama kutenda makosa chini ya sheria hii.
25. Uanachama wa vikundi vya kigaidi.
26. Kuandaa mikutano ya kuunga mkono vikundi vya kigaidi.
27. Kushiriki kutenda kosa la jinai chini ya sheria hii.

SEHEMU YA V
UPELELEZI WA MAKOSA YA JINAI

28. Mamlaka ya kukamata.
29. Mamlaka ya kupeleleza wakati wa dharura.
30. Mikusanyiko ya kijasusi.
31. Mamlaka ya kuingilia mawasiliano na kupokelewa mahakamani kwa mawasiliano yaliyoingiliwa.
32. Kushikilia ndege au chombo.
33. Mamlaka ya kuchukua mali iliyotumika kwenye mawasiliano ya kitendo cha kigaidi.

SEHEMU YA VI
UENDESHAJI WA MAKOSA

34. Mamlaka ya kusikiliza makosa ya jinai chini ya sheria hii.
35. Ushahidi kwa cheti.
36. Amri za kutwaa mali baada ya kutiwa hatiani chini ya Sheria hii.

SEHEMU YA VII
UREJESHWAJI NA USAIDIZI KATIKA MAMBO YA JINAI

37. Ubadilishanaji wa taarifa zinazohusiana na vikundi vya kigaidi na vitendo vya kigaidi.
38. Mikataba ya kupinga ugaidi kutumika kama msingi wa urejeshwaji.
39. Makosa yasiyochukuliwa kama ya kisiasa.

SEHEMU YA VIII
VIFUNGU MCHANGANYIKO

40. Wajibu wa kutoa taarifa zinazohusiana na makosa ya jinai na vitendo vya ugaidi.
41. Wajibu wa kutoa taarifa zinazohusiana na mali ya vikundi vya kigaidi au mali inayotumika kutendea makosa chini ya Sheria hii.
42. Amri za kukamata na kuzuia mali.
43. Amri za kutaifisha mali.
44. Kukataa maombi ya usajili na kufuta usajili wa wadhamini wanaohusiana na vikundi vya kigaidi.
45. Utoaji wa taarifa zinazohusiana na abiria katika ndege au chombo na watu wanaoingia au kuondoka nchini.

46. Mamlaka ya kuzuia kuingia na amri ya kuondoa watu.
47. Mamlaka ya kukataa maombi ya ukimbizi.
48. Mamlaka ya kutengeneza kanuni.

SEHEMU YA IX
MAREKEBISHO YATOKANAYO

49. Marekebisho katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985.
50. Marekebisho katika Sheria ya Usalama wa Taifa , 1970.
51. Marekebisho katika Sheria ya Urejeshwaji, 1965.
52. Marekebisho katika Sheria ya Mapato yatokanayo na Makosa ya Jinai, 1991.
53. Marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, 1995.
54. Marekebisho katika Sheria ya Ushahidi, 1967.

SURA YA 19

Sheria kwa ajili ya kutoa hatua thabiti za kupambana na ugaidi, kuzuia na kushirikiana na mataifa mengine katika kukomesha ugaidi na kueleza mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Imetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Sheria No. 21
Ya Mwaka 2002

[14 Disemba, 2002]
[Tangazo la serikali no ….. la …..]

SEHEMU YA I
VIFUNGU VYA UTANGULIZI

Jina Fupi
Sura ya 19

1.-(1) Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002, na itaanza kutumika tarehe ambayo Waziri husika ataitaja katika gazeti la Serikali.

Matumizi

2.-(1) Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

(2) Mtu yeyote atakayefanya kosa linaloadhibiwa chini ya Sheria hii nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atashughulikiwa na sheria hii kwa namna ile ile kana kwamba kosa hilo limetendeka katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tafsiri
Sura ya 19

3. Katika Sheria hii,labda muktadha uhitaji vinginevyo-

"Sheria " maana yake ni Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002;

“chombo cha usafiri angani" ni pamoja na ndege na helikopta;

"mawasiliano" maana yake ni mawasiliano yaliyopokelewa au yaliyotumwa kwa posta, simu ya upepo, simu au mawasiliano mengine yaliyopokelewa au kusafirishwaa kwa njia ya umeme, sumaku au njia nyingine;

“mtoa huduma ya mawasiliano" maana yake ni mtu anayetoa huduma au anapitisha au anapokea mawasiliano;

"Mahakama" maana yake ni Mahakama Kuu ya Tanzania, na kama muktadha utahitaji Mahakama Kuu ya Zanzibar;

Sheria Na. 12 ya1991

"Taasisi za fedha” maana yake ni benki ya biashara, taasisi nyingine yoyote inayotoa mikopo, karadha, vitega uchumi au inayokubali pesa inayowekwa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mabenki na Taasisi za fedha, 1991;

"kundi au chombo" maana yake ni mtu, kikundi, wadhamini, mfuko wa ubia au ushirika usiounganishwa au chama;

“Mkuu wa chombo" kuhusiana na chombo ina maana ya mmiliki au mtu ambaye kwa wakati huo anaongoza na kusimamia chombo hicho;

"waziri” maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya mambo ya ndani;

"mwendeshaji" kuhusiana na ndege ina maana ya mmiliki au mtu ambaye anaongoza na kusimamia ndege;

"afisa wa polisi" isipokuwa kama maelezo yatataka vinginevyo maana yake ni afisa wa polisi mwenye cheo cha au juu ya Mrakibu Msaidizi wa Polisi;

" mapato ya ugaidi" maana yake ni mali za aina zote ambazo zimepatikana kutokana na faida zinazotokana na vitendo vya kigaidi, ni pamoja na fedha taslimu bila ya kujali mali hizo ziko kwa jina la nani au ni nani amekutwa akizimiliki au kuwa na mamlaka nazo;

"mali" maana yake ni mali yoyote na rasilimali ya aina yoyote, iwe ni ya kuonekana au isiyoonekana, inayohamishika au isiyohamishika, inayoshikika au isiyoshikika na hati ya kumiliki na hati zinazoshuhudia umiliki wake, maslahi, mali hiyo au rasimali na pamoja na akaunti ya benki;

"kitendo cha kigaidi" maana yake ni kitendo au kutokutenda kunako elezewa katika kifungu cha 4 cha Sheria hii na neno "ugaidi" litatafsiriwa kwa mtazamo huu .

SEHEMU YA II
KUZUIWA KWA VITENDO VYA UGAIDI

Tafsiri na kuzuiwa kwa vitendo vya ugaidi.

4.-(1) Hapana mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nahapana raia wa Tanzania aishiye nje ya Jamhuri ya Muungano akayeruhusiwa kufanyakitendo cha kigaidi na mtu yeyote atakaye fanya hivyo atakuwa ametenda kosa la jinai.

(2) Mtu atatenda kosa la kigaidi ikiwa kwa nia ya ugaidi atatenda au hatatenda kitendo ambacho-

(a) kinaweza kufanya uharibifu mkubwa kwa nchi au shirika la kimataifa; au

(b) kimekusudiwa au kinaweza kusemekana kuwa kimekusudiwa-

(i) kutishia uma kwa kiwango kikubwa;

(ii) kuilazimisha Serikali kufanya au kutokufanya kitendo chochote;

(iii) kudhoofisha au kuharibu kwa kiwango kikubwa misingi ya kisiasa, kikatiba, kiuchumi au miundo ya kijamii ya nchi au shirika la kimataifa; au

(iv) kuishawishi Serikali hiyo au shirika hilo la kimataifa; au

(c) kinahusisha au kusababisha, kulingana na mazingira-

(i) shambulio kwa maisha ya mtu ambalolinaweza kusababisha kifo;

(ii) shambuliokwa uadilifu wa mtu;

(iii) utekaji wa mtu.

(3) Kitendo kitatafsiriwa kuwa ni ugaidi kwa mujibu wa Sheria hii ikiwa kitendo au tishio la kitendo ambacho-

(a) kinahusishai majeraha makubwa kwa mtu;

(b) kinahusishai uharibifu mkubwa wa mali;

(c) kinahatarisha maisha ya mtu;

(d) kinaasababisha hatari kubwa kwa afya au usalama wa uma au sehemu ya uma;

(e) kinahusisha utumiaji wa silaha za moto au milipuko;

(f) kinahusisha utolewaji kwenye mazingira au sehemu yake au kusambaza au kuiweka jamii au sehemu ya jamii katika-

(i) hatari yoyote, miali au viini hatarishi;
(ii) kemikali za sumu;
(iii) viumbe maradhia au ajenti wa kibaologia au sumu;

(g) kimeundwa aukimedhamiriwa kivuruge mifumo ya kompyuta au utoaji wa huduma inayohusiana moja kwa moja na mitambo ya mawasiliano, huduma za kibenki au za kifedha, usafiri au mitambo mingine muhimu;

(h) kimeundwa au kimedhamiriwa kuvuruga utoaji wa huduma muhimu za dharura kama vile polisi, ulinzi wa raia au huduma za kitabibu;

(i) kinahusisha kuleta hatari kwa usalama wa taifa au usalama wa uma, na kudhamiriwa , au kwa jinsi kilivyo, kinaweza kuonekana kuwa kimedhamiria -

(i) kuutisha uma au sehemu ya uma;

(ii) kuilazimisha Serikali au shirika la kimataifa kufanya au kuacha kufanya kitendo chochote, na kinatendwa kwa madhumuni ya kuonesha au kuunga mkono kitendo ambacho ni ugaidi kwa mujibu wa Sheria hii.

(4) Kitendo ambacho-

(a) kitavuruga huduma zozote;

(b) kimefanyika kuonyesha kupinga, kudhihirisha au kugoma kufanya kazi,

hakitachukuliwa kuwa ni kitendo cha ugaidi kwa mujibu wa kifungu hiki, ikiwa hakijadhamiriwa kuleta madhara yaliyotajwa katika aya, (a), (b), (c), au (d) ya kifungu kidogo cha (3).

(5) Katika Sheria hii , labda kama mazingira yatahitaji, vinginevyo, marejeo yoyote ya "kitendo cha kigaidi" yatajumuisha kitendo chochote kinachotajwa katika vifungu vya 5, 6, 7, 8, 9 na 10.

Kutenda kosa la mkutano wa kigaidi

5. Mtu atakuwa ametenda kosa ambaye-

(a) anapanga, anasimamia au anasaidia kupanga au kusimamia au kushiriki katika kikao au kitendo na hali akijua kuwa kitendo au kikao hicho kinahusiana na kitendo cha ugaidi;

(b) anatoa utaratibu au vifaa kwaajili ya mkutano au kwaajili ya kitendo na hali akijua kuwa kinahusiana na kitendo cha kigaidi; au

(c) anahudhuria mkutano na hali akijuakuwa unaunga mkono kikundi kilichopigwa marufuku au kutimiza malengo ya kikundi kilichopigwa marufuku.

Kosa la kikundi kilichopigwa marufuku kwaajili ya kitendo cha kigaidi

6. -(1) Pale ambapo watu wawili au zaidi wataungana, au pale kikundi kitajihusisha na kitendo chochote kwa lengo la--

(a) kushiriki au kusaidiana katika kitendo cha kigaidi;

(b) kuendeleza, kutumainisha au kulazimisha watu wengine kufanya kitendo cha kigaidi; au

(c) kupanga au kutenda vitendo vya kigaidi,

Waziri anaweza kutangaza kukipiga au kuwapiga marufuku kisheria watu hao au kikundi hicho.

(2) Mtu ambaye yuko au anadai kuwa katika kikundi kilichopigwa marufuku anatenda kosa la jinai.

(3) Utakuwa ni utetezi tosha kwa mtu atakayeshtakiwa chini ya kifungu

kidogo cha pili kuthibitisha kuwa kikundi ambacho anashitakiwa kuwa mjumbehakijatangazwa kupigwa marufuku wakati mtu huyo anayeshitakiwa alipokuwa mjumbe au alipotangaza kuwa mjumbe na kuwa hajashiriki kazi za kikundi hicho baada ya kutangazwa kupigwa marufuku.

Kusaidia ugaidi

7.-(I) Mtu atakuwa ametenda kosa ambaye, kwa namna yoyote -

(a) ataomba kusaidiwa au atasaidia kitendo cha kigaidi, au

(b) ataomba kusaidiwa au atasaidia, kikundi kilichopigwa marufuku.

(2) "Kusaidia" kama lilivyotumika katika kifungu kidogo cha (1) maana yake ni na itajumuisha -

(a) uchochezi unaosababisha ugaidi;

(b) kutoa msaada wa vifaa, silaha ambazo ni pamoja na za kibaiolojia, kikemichali au silaha za nyuklia, za kulipuka, mafunzo, usafiri, nyaraka au utambulisho wa uongo;

(c) kutoa msaada wa mawazo, ikiwa ni pamoja na kualika kuunga mkono kikundi kilichopigwa marufuku;

(d) Kutoa au kuwezesha huduma mfano za kifedha au huduma kama hizo zinazohusiana na gaidi, kikundi kinachojihusisha na kitendo cha ugaidi;

(e) Kushughulika moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja na mali ambayo inamilikiwa au kuongozwa na au kwa niaba ya gaidi yeyote pamoja na fedha zilizotokana na mali inayomilikiwa au kuendeshwa moja kwa moja na gaidi yeyote au kikundi kinachomilikiwa au kuongozwa na gaidi yeyote;

(f) kuingia au kusaidia moja kwa moja au kwa kificho katika mapatano ya kifedha yanayohusiana na mali iliyotajwa katika aya (e).

Kuhifadhi magaidi

8. Mtu anayemhifadhi, kumficha, au kusasbabisha ahifadhiwe au afichwe, mtu yeyote ambaye anamjua ametenda au ametiwa hatiani kwa kitendo chaa kigaidi, au mtu ambaye anajua ya kuwa hati ya kukamatwa au kufungwa kuhusiana na kitendo cha kigaidi imetolewa anatenda kosa.

Kumiliki kitu, habari nk kusiko ruhusiwa Sura ya 74

9.-(1) Mtu atakuwa ametenda kosa chini ya kifungu hiki ikiwa atakuwa anamiliki alama yoyote ya siri, neno la siri, mchoro, mpango, muhtasari au nyaraka yoyote, makala au taarifa zinazohusiana na au zinatumika katika sehemu zinazolindwa au kitu chochote katika eneo hilo kinyume na Sheria hii au Sheria ya Sehemu na Maeneo Yanayolindwa, 1969 au zilizokabidhiwa kwa mtu huyo kwa kuaminiwa na mtu mwenye dhamana na ofisi hiyo, au, alikuwa na nafasi ya kuingia au alipata au mtu huyo alikuwa na nafaisi ya kuingia kulingana na wadhifa au ofisi aliyoko au ni kama mtu ambaye ni au alikuwa na mkataba na serikali.

(2) Mtu atakayekuwa anamiliki kitu chochote kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) na ambaye -

(a) anatumia kitu hicho kwa madhumuni ya ugaidi au kwa madhumuni ambayo ni kinyume na usalama au maslahi ya Jamhuri ya Muungano; au

(b) Anawasilisha taarifa hizo kwa mtu yeyote mbali na mtu ambaye anamamlaka ya kuwasiliana naye au mtu ambaye kwa maslahi ya Jamhuri ya Muungano anapaswa kuwasiliana naye au;

(c) Kushidwa kuwa makini, au kujiweka katika mazingira ambayo yanahatarisha usalama wa taarifa hizo; au

(d) Anakaa na , mchoro, mpango, muhtasari au nyaraka yoyote, makala au taarifa wakati hana haki au ni kinyume na wajibu wake kufanya hivyo au ameshindwa kufuata maagizo halali kuhusiana na kurudisha au kuharibu

vitu hivyo; au

(e) anatumia kitu chochote kilichotajwa katika aya (a), (b), (c) au (d) kwa ajili ya ugaidi,

anatenda kosa chini ya Sheria hii.

(3) Mtu yeyote ambaye anapokea alama yoyote ya siri, neno la siri, mchoro, mpango, muhtasari au nyaraka yoyote, makala au taarifa huku akijua au akiwa na sababu za msingi kuamini kuwa wakati anapokea chochote kati ya hivyo kilikua kimefanyika ili kufanikisha au kuunga mkono kitendo cha kigaidi kinyume na vifungu vya sheria hii, isipokuwa kama itathibitika kuwa mawasiliano hayo yalikuwa kinyume cha matakwa yake, anatenda kosa.

Katazo dhidi ya vitisho vya vitendo vya kigaidi vya uongo

10.-(l) Hapana mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano na raia wa Tanzania nje ya Jamhuri ya Muungano atakayeruhusiwa kuwasiliana au kutoa kwa mtu mwingine taarifa kwa njia yoyote ambayo anajua au anaamini kuwa ya uongo kwa nia ya kumshawishi au kumshawishi mtu mwingine yeyote kuwa na imani ya uongo kuwa kitendo cha kigaidi kimefanyika, kinafanyika au kitafanyika.

(2) Mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano na raia yeyote wa Tanzania nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haruhusiwi kuweka kifaa au kitu chochote mahali popote pale kwa nia ya kumshawishi mtu kuwa na imani ya uongo kuwa-

(a) kifaa au kitu kinakaribia kulipuka au kuwaka moto na kusababisha madhara binafsi kwa mtu au uharibifu wa mali; au

(b) kifaa kina au kitu kina-

(i) vitu vyenye kuweza kuleta hatari, kudhuru, miali yenye uwezo wa kununurisha au kiini hatari;

(ii) kemikali zenye sumu; au

(iii) kiumbe maradhi chochote au wakala wa kibaolojia, au sumu ambayo inaweza kusababisha kifo, magonjwa au madhara kwa mtu au uharibifu wa mali.

(3) Mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano na raia yeyote wa Tanzania nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haruhusiwi kutuma kifaa au kitu chochote kwa njia ya posta, reli au kwa njia yoyote inayotumika kusafirisha vitu kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa nia ya kushawishi watu kuwa na imani ya uongo kuwa-

(a) kifaa au kitu kinakaribia kulipuka au kuwaka moto na kusababisha madhara kwa watu au kuharibu mali; au

(b) kitu kina au kifaa kina -

(i) vitu vya hatari, vya kudhuru au vyenye miali yenye uwezo wa kununurisha au kiini hatari;

(ii) kemikali zozote zenye sumu;

(iii) kiumbe maradhi chochote au wakala wa kibaolojia, au sumu ambayo inaweza kusababisha kifo, magonjwa au madhara kwa mtu au uharibifu wa mali.

(4) kwa ajili ya vifungu vidogo vya (1),(2) na (3), kutajwa kwa mtu anayeshawishi watu kuamini uongo hakuta hitaji mtu wa kwanza aliyetajwa kuwa na mtu maalum ambaye anataka kumshawishi kuwa na imani hiyo ya uongo.

Kipaumbele katika kutumika

11. Vifungu vya Sheria hii vitatumika hata kama vitakuwa ni kinyume na sheria nyingine yoyote zaidi ya sheria hii au hati rasmi yoyote inayotokana na Sheria nyingine yoyote.

SEHEMU YA III
VYOMBO MAALUM

Ugaidi wa kimataifa

12. -(1) Waziri anaweza kumtangaza mtu yeyote kuwa ni mtuhuhumiwa wa ugaidi wa kimataifa ikiwa-

(a) anasababu za msingi za kumshuku mtu huyo kuwa-

(i) anahusika au amehusika katika kutenda, kuandaa au kuchochea vitendo vya ugaidi wa kimataifa;

(ii) ni mwanachama wa jumuiya au kikundi cha kigaidi cha kimataifa;

(iii) anahusiana na kikundi cha kigaidi cha kimatifa na ana sababu za msingi kuamini kuwa mtu huyo ni hatari kwa usalama wa taifa;

(b) mtu huyo yuko kwenye orodha ya maazimiao ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa au hati ya jumuiya ya kimataifa kuwa ni muhusika wa vitendo vya kigaidi; au

(c) mtu huyo anachukuliwa na taifa hilo au jumuiya ya kimataiafa kuwa ni mtu ambaye anajishughulisha na vitendo vya ugaidi wa kimataifa.

(2) Pale ambapo Waziri atatoa tamko chini ya kifungu kidogo cha (1) (a), kwa namna ambayo ataona inafaa ataelekeza mtu aliyetangazwa kama ni mtuhumiwa wa ugaidi wa kimataifa ataarifiwe kwa jinsi ambavyo inawezekana.

(3) Waziri anaweza kutamka kikundi fulani kuwa ni cha ugaidi wa kimataifa ikiwa kikundi hicho-

(a) kinaongozwa au kushawishiwa na mtu aliye nje ya Jamhuri ya Muungano,na Waziri ana sababu za msingi kushuku kuwa kinahusika katika kutenda, kuandaa au kushawishi vitendo vya kigaidi vya kimatifa;au

(b) kiko kwenye orodha kama kikundi au jumuiya inayojishughulisha na vitendo vya kigaidi kulingana na Maazimio ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa au hati yoyote ya jumuiya ya kimataifa kama itakavyotolewa kila baada ya muda; au

(c) kinachukuliwa kuwa ni kikundi au jumuiya inayojishughulisha na vitendo vya kigaidi kama waziri atathibitisha na kutangaza katika *Gazeti*.

(4) Katika Sheria hii marejeo ya kikundi kilichopigwa marufuku kitachukuliwa kujumisha kikundi cha kigaidi cha kimataifa na pale inapoweza kutumika kwa mtuhumiwa wa ugaidi wa kimatifa.

(5) Kuhusiana na mtuhumiwa wa ugaidi wa kimaifa au kikundi cha ugaidi cha kimataifa, Waziri anaweza kutengeneza kanuni zitakazoeleza-

(a) kudhibiti fedha za huyo mtu au kikundi, mali au rasilimali zake nyingine za kiuchumi, ikiwa ni pamoja na fedha zilizotokana na mali, inayomilikiwa au kusimamiwa moja kwa moja au kwa kificho na yeye au kikundi au na watu wanaotumika kwa niaba yake au kwa niaba ya kikundi au kwa kufuata maelekezo yake au ya kikundi;

(b) kuzuia kuingia kwake au kwa kikundi au kupita katika Jamhuri ya

Muungano;

(c) kuzuia kusambaza moja kwa moja au kwa kificho ,kuuza na kuhamishia kwake au kwa kikundi zana za kivita, silaha, magari ya kivita na vifaa,vifaa vya kijeshi, vipuri na vifaa vinavyohusiana na hivyo, ushauri wa kiufundi,msaada au mafunzo yanayohusiana na shughuli za kijeshi moja kwa moja au kwa kificho;

(d) kuwa mtu yeyote atakayekwenda kinyume na kanuni yoyote iliyotengenezwa chini ya hiki kifungu kidogo anatenda kosa na atatumikia kifungo na kazi ngumu kwa kipindi kisichozidi miaka mitano..

(6) Kuhusiana na tamko lolote lililotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) na (3) waziri atatoa taarifa kwenye Gazeti na kwa namna nyingine kama atakavyoona inafaa.

(7) Katika kifugu hiki-

(a) "kitendo cha ugaidi wa kimataifa" kitatafsiriwa kumaanisha kitendo cha kigaidi kinachohusisha watu wasiokuwa raia; na

(b) "kikundi cha kigaidi cha kimataifa" kinamaanisha mtu au kikundi cha watu au jumuiya isiyo ya raia wa Tanzania au asili yake ni nje ya Tanzania na ambaye au ambacho kinatuhumiwa kutenda kosa lolote lililotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

SEHEMU YA IV
MAKOSA

Kutoa au kukusanya fedha kwa ajili ya kufanya ugaidi

13. Kila mtu anayetoa, au kukusanya kwa njia yoyote moja kwa moja au kwa kificho, fedha zozote, akidhamiria, akijua au akiwa na kila sababu za msingi kuamini kuwa fedha hizo au kiasi cha fedha zitatumika kufanikisha kitendo cha kigaidi anatenda kosa na akitiwa hatiani atatumikia kifungo kwa muda usiochini ya miaka kumi na tano na usiozidi miaka ishirini.

Kukusanya mali au kutoa mali na huduma kwaajili ya kutenda vitendo vya kigaidi

14. Kila mtu ambaye moja kwa moja anakusanya mali au anatoa, anakaribisha watu kutoa au kufanya mali au fedha au huduma zinazohusiana ziwepo-

(a) akidhamiria vitumike vyote au kiasi kwaajili ya kufanya au kurahisisha kutendeka kwa kitendo cha kigaidi au kwa lengo la kumnufaisha mtu yeyote anayetenda au kurahisisha kitendo cha kigaidi; au

(b) akijua kuwa vyote au kiasi vitatumika au vitanufaisha kikundi cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atumikia kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka ishirini na tano.

Kutumia mali kwaajili ya kutenda ugaidi

15. Kila mtu ambaye-

(a) anatumia mali moja kwa moja au kwa kificho, yote au sehemu tu ya mali hiyo, kwaajili ya kutenda au kurahisisha kutendeka kwa kitendo cha kigaidi; au

(b) anamiliki mali akiwa na nia kuwa itumike au akijua kuwa itatumika moja kwa moja au kwa kificho, yote au sehemu tu kwaajili ya kutenda au kurahisisha kutendeka kwa kitendo cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na kisichozidi miaka ishirini na tano

Mpango wa kubakisha au kutawala mali ya kigaidi

16. Kila mtu ambaye huku akijua ataingia au kuwa katika mpango utakao rahisisha kubakisha au kusimamia kwa mtu au kwaniaba ya mtu mwingine mali ya kigaidi -

(a) kwa kuficha,
(b) kwa kuindoa nje ya mamlaka ya nchi hiyo,
(c) kwa kuihamisha kwenda kwa mtu aliyependekezwa, au
(d) kwa njia nyingine yoyote,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na kisichozidi miaka ishirini na tano.

Kushughulika na mali inayomilikiwa au kusimamiwa na kikundi cha kigaidi

17.-(1) Kila mtu ambaye huku akijua-

(a) anajishughulisha moja kwa moja au kwa kificho na mali inayomilikiwa au kusimamiwa na au kwa niaba ya kikundi cha kigaidi;

(b) anaingia katika au kurahishisha moja kwa moja au kwa kificho mapatano ya kibiashara kuhusiana na mali iliyotajwa kwenye aya (a); au

(c) anatoa fedha au huduma nyingine kuhusiana na mali iliyotajwa katika aya (a) kufuata maelekezo ya kikundi cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka ishirini na tano na kisichozidi miaka thelathini na tano.

(2) Mtu ambaye kwa busara atachukua au hatachukua hatua ili kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) hata kuwa na hatia ya kijinai kwa kuchukua au kuacha kuchukua hatua ikiwa atathibitisha kuwa alichukua hatua za msingi na kujiridhisha kuwa mali inayohusika haikuwa inamilikiwa au kusimamiwa na au kwa niaba ya kikundi cha kigaidi.

Kushawishi na kuunga mkono vikundi vya kigaidi kwaajili ya kutenda vitendo vya kigaidi

18.-(1) Kila mtu ambaye anajua na kwa namna yoyote -

(a) atashawishi kuungwa mkono, au ataunga mkono kikundi chochote cha kigaidi ;au
(b) atashawishi kuungwa mkono au ataunga mkono kutendeka kwa kitendo cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini.

(2) Kwaajili ya aya (a) ya kifungu kidogo cha (1), ahadi yoyote ya kutoa au kutoa hati za kusafiria zilizo ghushiwa au za uongo kwa mwanachama wa kikundi cha kigaidi kinachukuliwa kuwa ni kuunga mkono kikundi cha kigaidi.

Kuhifadhi watu waliotenda vitendo vya kigaidi

19. Kila mtu ambaye anahifadhi au anaficha, anazuia au anaingilia ukamatwaji wa mtu mwingine yeyote hukuakijua au akiwa na sababu za kuamini kuwa mtu huyo-

(a) ametenda kitendo cha kigaidi; au

(b) ni mwanachama wa kikundi cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka kumi na nane na kisichozidi miaka thelathini.

20. Kila mtu ambaye huku akijua anaahidi kutoa au anatoa silaha yoyote kwa-

(a) kikundi cha kigaidi;

(b) mwanachama wa kikundi cha kigaidi;

(c) kwa mtu mwingine yeyote kwa ajili ya kutumia,au kwa manufaa ya kikundi cha kigaidi au mwanachama wa kikundi cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini.

Kuandikisha watu kuwa wanachama wa vikundi vya kigaidi au kushiriki katika vikundi vya kigaidi

21. Kila mtu ambaye huku akijua anakubali kumuandikisha au anamuandikisha mtu mwingine-

(a) kuwa mwanachama wa kikundi cha kigaidi; au

(b) kushiriki katika kutenda kitendo cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na kisichozidi miaka ishirini.

Kutangaza au kurahisisha kutendeka vitendo vya kigaidi katika taifa la kigeni

22. Kila mtu ambaye yuko katika Jamhuri ya Muungano-

(a) huku akijua anahamasisha au anarahisisha kufanyika kwa kitendo chochote katika taifa la kigeni kwa lengo la kufanikisha lolote kati ya malengo yafuatayo, iwe lengo limefanikiwa au la-

(i) kupinduliwa kwa kutumia nguvu au vurugu kwa serikali ya taifa hilo;

(ii) kusababisha kwa kutumia nguvu na vurugu uma katika taifa hilo la kigeni kuwa katika hofu ya kifo au kujeruhiwa;

(iii) kusababisha kifo au majeraha ya mwilini kwa mtu ambaye-

(a) ni mkuu wa taifa hilo la kigeni; au

(b) anasimamia au anafanya kazi zozote kwenye ofisi za serikali za taifa hilo la kigeni;

(iv) bila uhalali, kuangamiza au kuharibu mali yoyote inayomilikiwa na serikali ya taifa hilo la kigeni;

(b) anamuandikisha mtu mwingine kuwa mwanachamana au kutumikia katika nafasi yoyote kwenye kikundi cha watu ambacho malengo yake ni, au yanajumuisha malengo yaliyotajwa katika aya ya (a);

(c) anakusanya, analimbikiza au vinginevyo anahifadhi silaha zozote kwaajili ya kutenda kitendo chochote kilichotajwa katika aya (a);

(d) anafundisha au anatoa mafunzo , au anashiriki katika kutoa mafunzo kwa mtu yeyote jinsi ya kutumia silaha au kufanya mazoezi ya kijeshi kwaajili ya kumuandaa mtu huyo kufanya kitendo chochote kilichotajwa katika aya (a);

(e) anaruhusu kufundishwa jinsi ya kutumia silaha au kufanyishwa mafunzo ya kijeshi kwa lengo la kutenda kitendo chochote kilichotajwa katika aya (a);au

(f) anatoa fedha au vitu au anatoa huduma kwa mtu mwingine yeyote au kwa kikundi cha watu kwa lengo la kukuza au kuunga mkono kitendo chochote kilichotajwa katika aya (a);

(g) pokea au omba fedha au vitu u kutolewa kwa huduma kwaajili ya kutangaza au kuunga mkono kitendo chochote kilichotajwa katika aya (a),

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka ishirini na kisichozidi miaka thelathini.

Kuhamasisha makosa ya jinai

23. Kila mtu ambaye ni-

(a) mmiliki, mkazi, mpangaji au mtu anayesimamia jengo,chumba au sehemu yoyote, huku akijua anaruhusu mkutano wa watu kufanyika katika jengo,chumba au sehemu hiyo;

(b) mmiliki, mkodishaji wa meli, mpangaji, mwendeshaji, wakala, mkuu wa chombo au mmiliki,mkodishaji wa meli, mpangaji, mwendeshaji,wakala au rubani anayesimamia ndege huku akijua anaruhusu chombo au ndege kutumiwa,

kwaajili ya kutenda kosa au kusaidia au kuunga mkono kutendeka kwa kosa, anatenda kosa na akitiwa hatianiatahukumiwa kifungo kisichopungua miaka kumi na tano na kisichozidi miaka ishirini.

Kula njama kutenda kosa chini ya Sheria hii

24.-(1) Kila mtu anakayekula njama na mtu mwingine katika Jamhuri ya Muungano kufanya kitendo chochote nje ya Jamhuri ya Muungano, na kitendo hicho kingekuwa kimefanyika Tanzania kingekuwa ni kosa chini ya Sheria hii, atachukuliwa kuwa amekula njama za kutenda kitendo hicho katika Jamhuri ya Muungano.

(2) Kila mtu anayekula njama na mwingine iwe ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutenda kitendo chochote ndani ya Jamhuri ya Muungano kinachochukuliwa kuwa ni kosa chini ya Sheria hii, atachukuliwa kuwa amekula njama ndani ya Jamhuri ya Muungano kutenda kitendo hicho.

Uanachama katika vikundi vya kigaidi

25.-(1) Kila mtu ambaye-

(a) ni mwanachama;

(b) anatangaza kuwa ni mwanachama wa,

kikundi cha kigaidi, anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kutumikia kifungo kisichopungua miaka kumi na nane.

(2) itakuwa ni utetezi tosha kwa mtu anayeshitakiwa kwa kosa chini ya kifungu hiki kuthibitisha kuwa kikundi kinachosemekana kuwa alikuwa mwanachama wake sio kikundi cha kigaidi au katika tarehe ambayo-

(a) alikuwa mwanachama ;au

(b) alipotangaza kuwa mwanachama wa,

kikundi hicho au yeye hajashiriki katika shughuli zozote za kikundi hicho mara baada ya kuwa kikundi cha kigaidi.

Kupanga

26.-(1) Kila mtu anayepanga, anayeendesha au anayesaidia kupanga

mikutano ya kuunga mkono kikundi cha kigaidi

au kuendesha mkutano ambao anajua kuwa -

(a) ni wa kuunga mkono kikundi cha kigaidi;

(b) ni wakuendeleza shughuli za kikundi cha kigaidi;

(c) utahutubiwa na mtu ambaye ni au anatangaza kuwa yeye ni mwanachama wa kikundi cha kigaidi,

anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kutumikia kifungo kisichopungua miaka kumi na kisichozidi miaka kumi na tano.

(2) Katika kifungu hiki "mkutano" maana yake ni mkutano wa watu watatu au zaidi, iwe uma unaruhusiwa au la.

Kushiriki katika kutenda kosa chini ya Sheria hii

27. Kila mtu ambaye-

(a) anasaidia au anashawishi kutendeka;

(b) anajaribu;

(c) anakula njama kutenda;

(d) anashauri auanasababisha kutendeka kwa

kosa chini ya Sheria hii, anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kutumikia kifungo sawa sawa na kifungo cha kosa la kwanza kama lilivyotajwa .

SEHEMU YA V
UPELELEZI WA MAKOSA

Mamlaka ya kukamata

28.-(1) Afisa wa polisi yeyote anaweza kumkamata mtu yeyote aliyetenda kosa au anayetenda kosa au ambaye anasababu za msingi kumshuku kuwa ametenda kosa au anatenda kosa chini ya sheria hii bila hati ya kukamata.

(2) Kwa ajili ya kifungu kidogo cha (1) "afisa wa polisi" inamaanisha na inajumuisha afisa wa polisi wa au juu ya cheo cha mrakibu msaidizi, afisa uhamiaji au afisa usalama wa taifa la Tanzania.

Mamlaka ya kupeleleza wakati wa dharura Sura 20

29.-(1) Bila ya kuathiri vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa makosa ya Jinai, 1985 ikiwa kuna dharura na maombi ya kuomba hati ya kukamata mahakamani yatasababisha ucheleweshwaji unaoweza kuathiri usalama wa uma au utulivu, afisa polisi asiye chini ya cheo cha mrakibu msaidizi, mkuu wa kituo cha polisi, anaweza, bila ya kuzingatiaSheria nyingine yoyote, kwa msaada wa maafisa polisi wengine kama itakavyo lazimu-

(a) Kuingia na kupekua sehemu au eneo, ikiwa anasababu za kushuku kuwa ndani ya sehemu au eneo hilo-

(i) Kosa chini ya sheria hii linatendeka au linataka kutendeka; na

(ii) Kuna ushahidi kuwa kosa chini ya Sheria hii limetendeka;

(b) kumpekua mtu yeyote au gari litakalokutwa katika sehemu au eneo lolote ambalo amereuhusiwa kuingia na kupekua chini ya aya (a);

(c) kusimamisha, kupanda na kupekua chombo chochote, ndege au gari ikiwa ana sababu ya kushuku kuwa ndani ya hiyo ndege, gari au chombo kuna ushaidi wa kutendeka kwa kosa au kuna dalili kuwa huenda kosa chini ya Sheria hii limetendeka;

(d) kukamata,kuondoa na zuia kitu chochote ambacho kina au

kinaonekana kuwa na ushahidi wa kutendeka kwa kosa chini ya Sheria hii;

(e) kumkamata na kumshikilia mtu yeyote ambaye anamshuku kuwa ametenda au anataka kutenda kosa chini ya Sheria hii.

(2) Afisa wa polisi anaweza kutumia nguvu wakati akitekeleza mamlaka aliyopewa kwenye kifungu kidogo (1) pale inapolazimika.

(3) Mtu yeyote anayekutwa katika sehemu au eneo au chombo chochote, ndege au gari anaweza kushikiliwa na afisa wa polisi mpaka upekuzi chini ya kifungu kidogo (1) utakapomalizika.

(4) Endapo ushikiliwaji wa vitu, nyaraka na vitu vingine utafanyika chini ya kifungu hiki, orodha ya vitu vyote vilivyoshikiliwa, itawasilishwa mara moja.

(5) Kwa ajili ya kifungu hiki, kiasi cha nguvu ambacho kinaweza kutumika kisizidi vile inavyotakiwa.

(6) Afisa wa polisi ambaye atatumia nguvu kama itakavyolazimu kulingana na Sheria hii, hatakuwa na hatia katika shauri la jinai au la madai ikiwa kwa kutumia nguvu hiyo atasabaisha majeraha au kifo kwa mtu yeyote au uharibifu au kupotea kwa mali yoyote.

Mkusanyiko wa kijasusi

30.-(1) Kwaajili ya kuzuia au kugundua makosa ya ugaidi au kwaajili ya kuendesha mashitaka ya watuhumiwa chini ya sheria hii, Waziri anaweza ikiwa anaona ni lazima kutoa muongozo kuhusu-

(a) watoa huduma za mawasiliano kwa ujumla;

(b) watoa huduma za mawasiliano wa aina fulani;

(c) mtoa huduma ya mawasiliano fulani.

(2) Kabla ya kutoa muongozo chini ya kifungu hiki, waziri anaweza kushauriana na mtoa huduma ya mawasiliano yeyote atakaye muona anafaa.

(3) Muongozo katika kifungu hiki utaonyesha muda wa juu ambao mtoa huduma ya mawasiliano anaweza kuhitajika kuhifadhi taarifa za mawasiliano.

(4) Katika kifungu hiki-

"mtoa huduma ya mawasiliano" maana yake ni mtu anayetoa huduma ya posta, taarifa au mawasiliano, ikijumuisha mawasiliano ya simu na watoa huduma ya mtandao;

"taarifa" maana yake ni habari zilizorekodiwa katika hali ambayo zinaweza kutumiwa na kifaa kinachojiendesha chenyewe kikipewa maelekezo kwaajili hiyo.

(5) inapotokea kuna ukinzani, mahakama inaweza kwa maombi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kutoa amri inayomuelekeza mtoa huduma ya mawasiliano kufuata maagizo ya Waziri.

Mamlaka ya kuingilia mawasiliano na uwasilishwaji wa mawasiliano yaliyoingiliwa

31.-(l) Kulingana na kifungu kidogo cha (2), afisa wa polisi anaweza, kwaajili ya kupata ushahidi wa kutendeka kwa kosa chini ya sheria hii, kuiomba mahakama kutoa amri ya kuingilia mawasiliano.

(2) Afisa wa polisi anaweza kuiomba mahakama chini ya kifungu kidogo cha (1) ikiwa tu amepata ridhaa ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

(3) Mahakama ambayo maombi yamepelekwa chini ya kifungu kidogo

cha (1) inaweza kutoa amri-

(a) kumtaka mtoa huduma ya mawasiliano kuingilia na kuhifadhi mawasiliano yaliyotajwa au mawasiliano ya aina fulani yaliyopokelewa au kutumwa na huyo mtoa huduma ya mawasiliano;

(b) kumruhusu afisa wa polisi kuingia eneo lolote na kufunga kifaa chochote cha kuingilia na kuhifadhi mawasiliano maalum yaliyoelekezwa na kuondoa kifaa hicho katika eneo hilo,

ikiwa mahakama itaridhika kuwa ridhaa ya maandishi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepatikana kama inavyotakiwa kwenye kifungu kidogo cha (2) na kwamba kuna sababu za msingi za kuifanya iamini kuwa taarifa muhimu zinazohusiana na-

(i) kutendeka kwa kosa chini ya Sheria hii; au

(ii)habari za mtu anayeshukiwa na polisi kutenda kosa,

ziko katika mawasiliano hayo au mawasiliano ya aina hiyo.

(4) taarifa yoyote iliyoko kwenye mawasiliano-

(a) yaiyoingiliwa na kuhifadhiwa kulingana na amri chini ya kifungu kidogo cha (3);

(b) yaliyoingiliwa na kuhifadhiwa katika taifa la kigeni kulingana na sheria ya taifa hilo na kuthibitishwa na mahakama ya taifa hilo kuwa iliingiliwa na kuhifadhiwa,

itapokelewa katika mashauri ya makosa chini ya Sheria hii kama ushahidi wa ukweli wa yaliyomo bila ya kujali kuwa ina fununu.

Kuzuiwa kwa ndege au chombo

32.-(1) Mkuu wa Jeshi la Polisi anaweza kutoa amri ya kuzuiwa kwa ndege au chombo ikiwa anaona kuwa-

(a) tishio limetolewa la kufanyika kwa kitendo cha ghasia dhidi ya ndege au chombo au dhidi ya mtu au mali iliyoko kwenye ndege au chombo hicho; au

(b) kitendo cha ghasia kinataka kutendeka dhidi ya ndege au chombo au dhidi ya mtu yeyote au mali iliyoko kwenye ndege au chombo hicho.

(2) Pale mwendeshaji wa ndege au chombo anaposhindwa kufuata amri ya kuzuiwa chini ya kifungu kidogo cha (1), mtu aliye na mamlaka anaweza-

(a) kuingia au kumruhusu mtu yeyote kuingia kwenye ndege au chombo;

(b) kupanga ili kumuondoa mtu au kitu kutoka kwenye ndege au chombo,

na anaweza kutumia nguvu ya kawaida au kumruhusu mtu mwingine kutumia nguvu ya kawaida kwa ajili hiyo.

(3) Mtu atakaye ruhusiwa atatoa taarifa kwa mwendeshaji wa ndege au chombo kuhusu amri ya kuzuiliwa iliyotolewa chini ya kifungu hiki.

(4) Pale ambapo mwendeshaji wa ndege au chombo atapinga amri ya kuzuiwa Waziri anaweza kutoa amri ya kubadilisha au kufuta amri baada ya kusikiliza pande zinazohusika.

(5) mtu yeyote ambaye-

(a) bila sababu za msingi, anashindwa kufuata maelekezo ya amri ya kuzuiwa; au

(b) kwa makusudi anapinga au anamzuia mtu yeyote anayetenda kulingana na kifungu kidogo (2),

anatenda kosa.

(6) Kwaajili ya kifungu hiki, Waziri anaweza, kwa maandishi, kumteua mtu anayeona anafaa kuwa mtu mwenye mamlaka.

Mamlaka ya kutwaa mali iliyotumika kwenye vitendo vya kigaidi

33.-(1) Pale Mkuu wa jeshi la Polisi au Kamishna wa Polisi anakuwa na sababu za msingi za kushuku kuwa mali yoyote imekuwa ikitumika au inatumika kutendea kosa chini ya Sheria hii, anaweza kutwaa mali hiyo.

(2) Mkuu wa Jeshi la Polisi au Kamishna wa Polisi anaweza kutumiamamlaka yake chini ya kifungu kidogo cha (1), kuhusiana na mali hiyo iwe kuna mashauri yaliyofunguliwa chini ya Sheria hii au la.

(3) Kamishna wa Polisi kwa haraka iwezekanavyo baada ya kutwaa mali yoyote chini ya kifungu kidogo cha (1) anaweza kufanya maombi ya upande mmoja mahakamani kwaajili ya kuomba amri ya kuzuia kuhusiana na mali hiyo.

(4) Mahakama ambayo maombi yamefanyika chini ya kifungu kidogo (3) kuhusiana na mali iliyotajwa kwenye maombi haitatoa amri ya kuzuia isipokuwa kama mtu huyo-

(a) amempa kila mtu anayehusika fursa ya kusikilizwa; au

(b) anasababu za msingi za kuamini kuwa mali hiyo imetumika au inatumika kutendea kosa chini ya Sheria hii.

(5) kulingana na kifungu kidogo cha (6), kila amri ya kuzuia itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (4) itakuwa halali kwa muda wa siku sitini na inaweza, kwa maombi kutolewa tena na mahakama kwa muda wa siku sitini nyingine mpaka mali iliyotajwa kwenye amri itakapopelekwa mahakamani katika shauri kwaajili ya kosa chini ya sheria hii kuhusu mali hiyo.

(6) Mahakama inaweza kuachia mali yoyote iliyozuiwa na amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo (4) ikiwa -

(a) hakuna tena sababu za msingi kushuku kuwa mali imekuwa ikitumika au ilitumika kutenda kosa chini ya Sheria hii, au

(b) hakuna mashauri yaliyofunguliwa mahakamani ndani ya miezi sita kwa kosa chini ya Sheria hii kuhusiana na mali hiyo.

(7) Kutwaliwa kwa mali yoyote na afisa wa polisi chini ya kifungu kidogo cha (1) haitachukuliwa kuwa ni kwenda kinyume na kifungu cha 8.

(8) Mashauri ya madai na jinai hayatafunguliwa dhidi ya afisa wa polisi kwasababu ya kutwaa mali kwa nia njema kulingana na kifungu kidogo cha (1).

SEHEMU YA VI
KUSIKILIZWA KWA KESI

Mamlaka ya kusikiliza kesi chini ya Sheria hii

34.-(1) Mahakama Kuu itakuwa na mamlaka ya kusikiliza makosa chini ya Sheria hii.

(2) Mashitaka chini ya Sheria hii hayatafunguliwa mpaka ridhaa ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai itakapopatikana.

(3) Mahakama inaweza kwa kuombwa na au kwaniaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai kutoa amri kuwa mtu yeyote asichapishe-

(a) jina, anwani au picha ya shahidi yeyote katika kesi yoyote inayosikilizwa au inayotaka kusikilizwa mbele yake kwa kosa lolote chini ya Sheria hii; au

(b) ushahidi wowote au mambo yoyote yanaweza kumtambulisha shahidi.

(4) Mahakama inaweza, kwa kuombwa na au kwa niaba ya Mkurugenzi wa Mashtaka ya Jinai, kwa usalama au utulivu wa taifa, kuwaondoa katika kesi hiyo watu wengine zaidi ya wahusika na wawakilishi wao kisheria.

(5) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na amri itakayotolewa chini ya kifungu kidogo (3) atakuwa ametenda kosa.

(6) Kwaajili ya kifungu kidogo cha (2) kitendo au kutokutenda kitendo nje ya Jamhuri ya Muungano na kama kitendo hicho kingefanyika ndani ya Jamhuri ya Muungano kingekuwa kosa chini ya sheria hii kitachukuliwa kuwa kama kimefanyika ndani ya jamhuri ya Muungano ikiwa mtu aliyetenda kitendo au kuacha kutenda kitendo hicho yupo ndani ya Jamhuri ya Muungano na hawezi kupelekwa kwenye taifa la kigeni ambalo lina mamlaka juu ya kosa hilo.

Ushahidi wa Cheti

35. Katika shauri lolote kwa kutenda kosa chini ya Sheria hii, suala likiibuka kuhusu ikiwa kitu chochote ni silaha, cha hatari, miali ya nguvu au viini hatarishi, kemikali za sumu au vijiumbe maradhi au viini vya kibaiolojia au sumu, cheti kilichosainiwa na mamlaka inayohusika kikithibitisha kuwa kitu hicho ni silaha, cha hatari, miali ya nguvu au ni viini hatarishi, kemikali za sumu au vijiumbe maradhi au viini vya kibaiolojia au sumu kitapokelewa kama ushahidi bila ya uthibitisho wa saini au mamlaka ya mtu ambaye anayeonekana kusaini na kukiwa hakuna ushahidi wa kupinga kitakuwa ni uthibitisho wa kilichoandikwa humo.

Amri za kutaifisha mali baada ya kutiwa hatiani kwa makosa chini ya Sheria hii

36.-(1) Ikiwa mtu yeyote atatiwa hatiani kwa kosa chini ya Sheria hii, Mahakama inaweza kutoa amri ikitaka mali yoyote-

(a) iliyotumika au kuhusiana na; au

(b) kupokelewa kama malipo au tuzo ya,

kutenda kosa, itaifishwe na kuwa mali ya Jamhuri ya Muungano

(2) Kabla ya kutoa amri chini ya kifungu kidogo (1), mahakama itampa kila muhusika wa mali ambayo inataka kutolewa amri fursa ya kusikilizwa.

(3) Mali iliyotaifishwa na Jamhuri ya Muungano chini ya kifungu kidogo(1), itakuwa ya Serikali-

(a) ikiwa hakuna rufaa iliyokatwa dhidi ya amri hiyo ndani ya muda ambao rufaa inaweza kukatwa , na

(b) ikiwa rufaa imekatwa dhidi ya amri hiyo, mpaka maamuzi ya rufaa hiyo yatakapotolewa .

SEHEMU YA VII
KUREJESHWA NA MSAADA KWENYE MAMBO YA JINAI

kubadilishana taarifa zinazohusu vikundi vya kigaidi na vitendo vya kigaidi

37. Mkuu wa Jeshi la Polisi au Kamishna wa Polisi anaweza, anapoombwa na mamlaka husika ya taifa la nje kutoa taarifa aliyokuwa nayo au iliyokuwa kwa idara au wakala nyingine za Serikali kuhusiana na-

(a) vitendo au mienendo ya vikundi vya kigaidi au watu wanaoshukiwa kujihusisha na kutenda vitendo vya kigaidi;
(b) kutumia nyaraka za kusafiria za kughushi au za uongo za watu wanaoshukiwa kujihusisha kutenda vitendo vya kigaidi;
(c) kuvusha silaha na vifaa nyeti kunakofanywa na vikundi vya kigaidi au watu wanaoshukiwa kujihusisha na kutenda vitendo vya kigaidi; au
(d) kutumiwa kwa tekinolojia ya mawasiliano na vikundi vya kigaidi,

ikiwa kutoa huko kwa taarifa hakuzuiliwi na kifungu chochote cha sheria na kwa busara ya Mkuu wa Jeshi la Polisi au Kamishna wa Polisi hakutakuwa na madhara kwa utulivu au usalama wa taifa.

Mikataba ya kupinga ugaidi kutumika kama sababu ya urejeshwaji Sura 368

38.-(1) Ikiwa Jamhuri ya Muungano itakuwa sehemu ya mkataba wa kimataifa wa kupinga ugaidi na pakawepo mpango wa urejeshwaji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taifa lingine ambalo ni sehemu kwenye mkataba wa kupinga ugaidi, kwa ajili ya Sheria ya Urejeshwaji ya mwaka 1965, mpango wa urejeshwaji utachukuliwa kwaajili ya Sheria ya Urejeshwaji kujumuisha vifungu vya urejeshwaji kuhusiana na makosa yanayoangukia kwenye mkataba wa kupinga ugaidi.

(2) Ikiwa Jamhuri ya muungano wa Tanzania ni sehemu ya mkataba wa kupinga ugaidi na hakuna mpango wa urejeshwaji kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taifa lingine ambalo ni sehemu ya mkataba wa kupinga ugaidi, Waziri anaweza kwa amri itakayochapishwa kwenye Gazeti kuchuchukulia mkataba wa kupinga ugaidi kwaajili ya Sheria ya Urejeshwaji kama ni mpango wa urejeshwaji kati ya Jamhuri ya Muungano na taifa hilo kufanya urejeshwaji kuhusiana na makosa yaliyomo kwenye mkataba wa kupinga ugaidi.

Makosa ambayo hayatachukuliwa kama ya kisiasa Sura ya 368

39. Bila ya kuathiri kitu chochote kwenye Sheria ya Urejeshwaji ya mwaka 1965 kosa linalosababisha;

(a) kifo au majeraha makubwa kwa mtu; au
(b) uharibifu mkubwa wa mali,

kwa ajili ya urejeshwaji chini ya Sheria hii, utachukuliwa kuwa si kosa lenye mwelekeo wa kisiasa au kosa linalohusiana na kosa la kisiasa au kosa lililochochewa kwa nia za kisiasa.

SEHEMU YA VIII
VIFUNGU MCHANGANYIKO

Wajibu wa kutoa taarifa zinazohusiana na makosa na vitendo vya

40.-(1) Kila mtu ambaye atakuwa na taarifa ambazo zinaweza kusaidia katika-

kigaidi

(a) kuzuia kutendwa kwa kosa la kigaidi na mtu mwingine;

(b) kukamatwa au kushitakiwa kwa mtu mwingine kwa kosa chini ya Sheria hii,

atatakiwa mara moja atoe taarifa kwa afisa wa polisi wa cheo kisicho chini ya mrakibu msaidizi wa polisi au kwa mkuu wa kituo.

(2) Kifungu kidogo cha (1) hakihitaji kutolewa kwa taarifa ambayo inalindwa na upendeleo.

(3) Mashauri ya Jinai na madai hayatafunguliwa kwa mtu yeyote kwa kutoa taarifa kwa nia njema kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (1).

(4) Mtu yeyote ambaye atashindwa kufuata kifungu kidogo (1) anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kutumikia kifungo kisichopungua miaka miwili nakisichozidi miaka mitano.

Wajibu wa kutoa taarifa zinazohusiana na mali ya vikundi vya kigaidi au mali inayotumika kwaajili ya kutenda vitendo vya kigaidi chini ya Sheria hii.

41.-(1) Kila mtu atatakiwa kutoa taarifa haraka kwa afisa wa polisi kuhusiana na-

(a) kuwepo kwa mali iliyo chini ya usimamizi wake au anayoisimaia, na ambayo anajua inamilikiwa au inasimamiwa na, au kwa niaba ya kikundi cha kigaidi;

(b) taarifa yoyote inayohusu mapatano au matarajio ya mapatano kuhusu mali yoyote iliyotajwa katika aya (a).

(2) Kila taasisi ya fedha itatakiwa kutoa taarifa kila baada ya miezi mitatu kwa afisa polisi na kwa chombo chochote chenye mamlaka ya kuongoza na kusimamia kazi zake-

(a) kwamba haimiliki au haisimamiimali yoyote inayomilikiwa au kusimamiwa na au kwa niaba na kikundi cha kigaidi;

(b) kwamba inamiliki au inasimamia mali hiyo, pamoja na taarifa zinazohusiana na watu, akaunti za bank, na miamala inayohusika na thamani ya mali hizo.

(3) Kwa kuongeza mahitaji ya kifungu kidogo cha (2), kila taasisi ya fedha itatakiwa kutoa taarifa kwa afisa wa polisi kuhusu kila muamala unaotokea wakati wa uendeshaji wa kazi zake na ambapo kuna sababu za msingi za kushuku kuwa muamala huo unahusiana na kutendeka kwa kitendo cha kigaidi.

(4) Mashauri ya Jinai na madai hayatafunguliwa dhidi ya mtu yeyote kutokana na kutoa taarifa kwa nia njema kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (1) au (2) au (3).

(5) Mtu yeyote ambaye anashindwa kufuata kifungu kidogo (1), (2) au (3), anatenda kosa na akitiwa hatiani atahukumiwa kutumikia kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili.

Amri za kukamata au kuzuia mali

42. -(1) Pale ambapo Mahakama itaridhika kutokana na maombi ya upande mmoja kuwa kuna sababu za msingi kuamini kuwa katika jengo lolote,mahali au chombo kuna mali ambayo amri ya kutaifisha inaweza kutolewa chini ya kifungu cha 43, mahakama itatoa-

(a) hati inayomruhusu afisa wa polisi kupekua jengo, mahali au chombo na kuikamata mali hiyo kama itapatikana na mali nyingine yoyote ambayo afisa wa polisi anaamini kuwa kuna sababu za msingi kuwa amri chini ya kifungu cha 43 inaweza kutolewa dhidi yake;

(b) amri inayokataza mtu yeyote kuharibu au kushughulika na mali

hiyo zaidi ya vile ilivyoelezwa kwenye amri.

(2) Kwa maombi yatakayofanyika chini ya kifungu kidogo (1) Mahakama inaweza, kwa ombi la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ikiwa mahakama itaona hali inataka-

(a) kumchagua mtu kusimamia na kuongoza au kushughulika na mali yote au sehemu yake, kulingana na maelekezo ya Mahakama;

(b) kumtaka mtu yeyote anayemiliki mali hiyo kutoa umiliki wa mali hiyo kwa mtu aliyechaguliwa chini ya aya (a).

(3) Mamlaka ya kuongoza au kushughulika na mali chini ya kifungu kidogo cha (2) itajumuisha-

(a) Kuhusiana na mali inayoharibika kwa haraka au kushuka thamani yake haraka, mamlaka ya kuuza mali hiyo, na

(b) Kuhusiana na mali iliyo na thamani kidogo au isiyo na thamani kabisa, mamlaka ya kuharibu mali hiyo.

(4) Kabla ya mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (2) hajaharibu mali iliyotajwa kwenye kifungu kidogo (3) (b) ataiomba mahakama itoe amri ya kuharibu.

(5) Kabla ya kutoa amri ya kuharibu mali yoyote Mahakama itataka taarifa itolewe kwa namna ambayo Mahakama itaagiza, kwa mtu yeyote ambaye kwa maoni ya Mahakama kuwa anahusika na mali hiyo na itampa mtu huyo fursa ya kusikilizwa.

(6) Mahakama inaweza kutoa amri kuruhusu mali ambayo maombi ya kuiharibu yamefanywa chini ya kifungu kidogo cha (4) iharibiwe ikiwa Mahakama itajiridhisha kuwa mali hiyo ina thamani ndogo au haina thamani yoyote ya kifedha.

(7) Amri ya kuongoza chini ya kifungu kidogo (2), itaisha kuwa na nguvu ikiwa mali ambayo ni kiini cha amri ya kuongoza itarudishwa kwa muombaji kulingana na sheria au itataifishwa na Jamhuri ya Muungano.

(8) Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kuiomba Mahakama kufuta au kubadilisha hati au amri iliyotolewa chini ya kifungu hiki wakati wowote.

Amri za kutaifisha mali

43-(1) Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutuma maombi Mahakamani kuomba amri ya kutaifisha kuhusiana na-

(a) Mali inayomilikiwa au kusimamiwa na au kwa niaba ya kikundi cha kigaidi; au

(b) Mali iliyotumika, inayotumika au itakayotumika yote au kiasi kutenda au kurahisisha kutendeka kwa kitendo cha kigaidi.

(2) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatakiwa kuweka majina ya wajibu maombi katika maombi yaliyofanyika chini ya kifungu kidogo (1) watu wale tu ambao wanajulikana kumiliki au kusimamia mali ambayo ni kiini cha maombi.

(3) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa taarifa ya maombi chini ya kifungu kidogo cha (1) kwa wajibu maombi waliotajwa kwenye maombi kwa namna ambayo Mahakama itaagiza.

(4) Ikiwa Mahakama itaridhika kwa ulingano wa kawaida kuwa mali ambayo ni kiini cha maombi ni mali iliyotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) (a) au (b), itaamuru kuwa mali hiyo itaifishwe na kushughulikiwa kama

itakavyo agizwa na Mahakama.

(5) Ikiwa Mahakama itakataa maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo (1) Jaji atatoa amri itakayoelezea mali na kutangaza kuwa si mali iliyotajwa katika kifungu kidogo hicho.

(6) Kwa maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), Mahakama inaweza kutaka taarifa kupelekwa kwa mtu yeyote ambaye kwa mtazamo wa Mahakama anaonekana kuwa na maslahi katika mali hiyo na mtu huyoatakuwa na haki yakujumuishwa kama mjibu hoja ya maombi.

(7) Ikiwa mahakama itaridhika kuwa mtu aliyetajwa katika kifungu kidogo (6)-

(a) Ana maslahi katika mali ambayo ni kiini cha maombi;

(b) Ametumia umakini wa kutosha kuhakikisha mali haingetumika kutendea au kurahisisha kutendeka kwa kitendo cha kigaidi; na

(c) Sio mwanachama wa kikundi cha kigaidi,

Mahakama itatoa amri kuwa maslahi yake yasiathiriwe na amri na itatangaza aina na kiwango cha maslahi hayo.

(8) Mtu yeyote anayedai kuwa anamaslahi na mali ambayo imetaifishwa na hajapewa taarifa chini ya kifungu kidogo cha (6), anaweza kupeleka maombi mahakamani kubalisha au kuondoa amri iliyotolewa chini ya kifungu kidogo (4) sio zaidi ya siku sitini tangu kutolewa kwa amri ya kutaifishwa.

(9) Wakati wa kusubiri maamuzi ya rufaa dhidi ya amri ya kutaifishwa iliyotolewa chini ya kifungu hiki, mali iliyozuiwa chini ya kifungu cha 42 itaendelea kuzuiwa, mali iliyokamatwa kwa hati iliyotolewa chini ya kifungu hiki itendelea kushikiliwa na mtu yeyote aliyeteuliwa kuitawala, kuisimamia au kuishughulikia mali hiyo chini ya kifungu hicho ataendelea kufanya hivyo.

(10) Maelezo ya kifungu hiki hayataathiri utekelezaji wa vifungu vingine vya Sheria hii kuhusu utaifishwaji wa mali.

Kukataa maombi ya kusajiliwa na kufutwa kwa usajili wa wadhamini wenye uhusiano na vikundi vya kigaidi

44.-(1) Waziri anaweza kusaini cheti kikieleza kwa mtazamowake „kwa taarifa aliyoipokea pamoja na taarifa za kiusalama au za kiinteligensia, kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kuwa chombo kinachoomba usajili wa wadhamini kimefanya,kinafanya, au kinataka kufanya ili kuwezesha upatikanaji wa moja kwa moja au wa kificho kwa nyezo zozote kwa kikundi cha kigaidi.

(2) Baada ya kusaini cheti chini ya kifungu kidogo cha (1), Waziri au mtu aliyeruhusiwa na yeye atahakikisha muombaji au wadhamini waliosajiliwa wamepewa wao wenyewe mkononi au kwa barua iliyosajiliwa na kutumwa kwenye anwani yao nakala ya cheti na taarifa inayoeleza kuwa cheti kitapelekwa Mahakamani sio kabla ya siku saba baada ya kupewa kwao taarifa na ikiwa cheti kitaonekana kinafaa, muombaji hatakuwa na sifa ya kusajiliwa kama wadhamini waliosajiliwa au usajili wa wadhamini waliosajiliwa wa amana utafutwa kama itakavyokuwa.

(3) Cheti au kitu chochote kinachotokana nacho hakitatakiwa kupitiwa au kuzuiwa, kukatazwa, kutoondolewa, kufutwa au kufanyiwa kitu chochote isipokuwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(4) Siku saba baada ya kupelekewa kwa mujibu wa kifungu (2) au

kwa haraka iwezekanavyo baada ya hapo, Waziri au mtu aliyeruhusiwa na yeye atatakiwa-

(a) kuandikisha nakala ya cheti katika mahakama kwaajili ya uamuzi chini ya kifungu kidogo cha (5); na,

(b) kufanikisha muombaji au wadhamini waliosajiliwa wanapelekewa, wao wenyewe au kwa barua iliyosajiliwa kwa anwani waliyoitumia mara ya mwisho pamoja na taarifa inayowajulisha kuhusu kuandikishwa kwa cheti.

(5) Baada ya kuandikisha cheti mahakamani chini ya kifungu kidogo (4), mahakama -

(a) itapitia katika ofisi ya mahakama taarifa pamoja na ripoti za kiusalama au jinai au kijasusi zilizopitiwa na Waziri kabla ya kusaini cheti na kusikiliza ushahidi wowote au taarifa na kwa maombi ya waziri, kusikiliza ushahidi wote au sehemu `bila ya uwepo wa waombaji au wadhamini waliosajiliwa, na ikiwa Mahakama itaona kuwa kutoa taarifa kutaathiri usalama wa taifa au kuhatarisha usalama wa mtu yeyote;

(b) itampa mwombaji au chombo cha hisani kilicho sajiliwa taarifa itakayotoa kwa ufupi taarifa zilizoko Mahakamani ili kuwawezesha waombaji au chombo cha hisani kilicho sajiliwa kuelezwa mazingira yaliyopelekea cheti bila ya kueleza taarifa ambazo kutolewa kwake kwa mtazamo wa Mahakama utaathiri usalama wa taifa au utahatarisha usalama wa mtu yeyote;

(c) itampa muombaji au chombo cha hisani kilichosajiliwa fursa ya kusikilizwa; na

(d) itaamua kama cheti kinafaa kwa kuangalia taarifa zilizoko Mahakamani na kama ikiona hakifai, kukifuta.

(6) Pale ambapo Mahakama chini ya kifungu kidogo cha (5) itaamua kuwa kuna sababu ya cheti kutolewa, waziri atasababisha cheti kichapishwe kwenye Gazeti.

(7) Cheti kitakachoamuliwa kuwa kinasababu ya msingi chini ya kifungu cha (5) kitachukuliwa kuwa ni sababu ya msingi kwa kukataa maombi ya kusajili chombo cha hisani kilichotajwa kwenye cheti au kufutwa kwa chombo cha hisani kilicho sajiliwa kilichotajwa kwenye cheti.

Kutolewa kwa taarifa zinazohusu abiria wa chombo na ndege walioingia au kuondoka katika nchi

45 –(1) Kwa–

(a) mwendesha ndege au kiongozi wa chombok inachoondoka kutoka Jamhuri ya Muungano; au

(b) mwendesha ndege iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano au muongoza abiria wa chombo kilichosajiliwa katika Jamhuri ya Muunganoanayeondoka kutoka sehemu yoyote nje ya Jamhuri ya Muungano,

kwa mujibu wa kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu kidogo cha (5) anaweza kutoa-

(i) kwa afisa polisi taarifa yoyote aliyonayo inayohusu watu walioko au wanaotegemea kuwa kwenye ndege au chombo kama itakavyokuwa; na

(ii) kwa mamlaka inayohusika ya taifa la nje taarifa aliyo nayo na ambayo inatakiwa kwa mujibu wa sheria za taifa hilo la kigeni inayohusu watu walioko au wanaotegemea kuwa kwenye ndege au chombo kama itakavyokuwa.

(2) Mkugenzi wa Uhamiaji kulingana na kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu kidogo cha (5) anaweza kutoa taarifa zozote alizonazo na zinazohitajika kwa mujibu wa sheria za taifa hilo la kigeni, zinazohusu mtu aliyeingia au kuondoka katika Jamhuri ya Muungano kwa njia ya nchi kavu kwa mamlaka inayohusika.

(3) Kutolewa kwa taarifa zozote chini ya kifungu kidogo cha (1) au (2) kulingana na kanuni zilizotengenezwa chini ya kifungu kidogo cha (5) zitachukuliwa kuwa si uvunjifu wa kifungu chochote cha sheria kinachozuia kutolewa kwa taarifa.

(4) Taarifa iliyotolewa kwa afisa wa polisi chini ya kifungu kidogo cha (1) haitatumiwa au kutolewa na Mkurugenzi wa Uhamiaji isipokuwa kwa dhumuni la usalama wa taifa au umma.

(5) Waziri anaweza kutengeneza kanuni muhimu ili madhumuni ya kifungu hiki yaweze kufikiwa, pamoja na kanuni-

(a) zinazohusu aina au tabaka za taarifa ambazo zinaweza kutolewa chini ya kifungu hiki;

(b) zinazotaja mataifa ya kigeni ambayo yanaweza kupewa taarifa.

Mamlaka ya kuzuia kuingia na kutoa amri ya kuondoa watu

46.-(1) Mkurugenzi wa Uhamiaji au afisa mwingine aliyeruhusiwa chni ya sheria zinazohusu uhamiaji hatatoa idhini au mamlaka mengine ya kumruhusu mtu kuingia katika Jamhuri ya Muungano ikiwa anasababu za msingi kuamini kuwa mtu huyo amekuwa, anajihusisha au atajihusisha kutenda kitendo vya kigaidi.

(2) Pale ambapo waziri wa Uhamiaji anasababu za msingi kuamini kuwa kuna mtu ndani ya Jamhuri ya Muungano ambaye amekuwa, anajihusisha au atajihusisha kutenda kitendo vya kigaidi, anaweza kutoa amri ya kumtaka mtu huyo kuondoka katika Jamhuri ya Muungano na kuendelea kukaa nje ya Jamhuri ya Muungano

(3) Mtu ambaye amri chini ya kifungu kidogo cha (2) imetolewa dhidi yake ataondoka kutoka Jamhuri ya Muungano na ataendelea kukaa nje ya Jamhuri ya Muungano ilimradi amri hiyo bado ipo hai.

(4) Mtu ambaye amri chini ya kifungu kidogo cha (2) imetolewa dhidi yake anaweza kushikiliwa kwa namna ambayo Waziri ambaye anashughulikia uhamiaji ataelekeza na anaweza kuwekwa kwenye chombo au ndege inayoondoka kutoka Jamhuri ya Muungano.

Mamlaka ya kukataa maombi ya ukimbizi

47. Waziri anayeshughulikia uhamiaji anaweza, baada ya kuangalia usalama wa taifa na umma, kukataa maombi ya mtu yeyote anayeomba kupata hadhi ya ukimbizi ikiwa anasababu za msingi kuamini kuwa muombaji ametenda au anataka kutenda kitendo cha kigaidi.

Mamlaka ya kutengeneza kanuni

48.-(1) Waziri anaweza kutengeneza kanuni zinazohusu mambo yote ambayo yanatakiwa au yanaruhusiwa kutengenezwa kanuni chini ya Sheria hii.

(2) Kwa kutegemea kifungu kidogo cha (3), kila kanuni itakayotengenezwa chini ya kifungu kidogo cha (1), itachapishwa kwenye gazeti na itaanza kutumika siku iliyochapishwa au siku nyingine kama itakavyoelezwa kwenye kanuni.

(3) Kila kanuni itakayotengenezwa chini ya kifungu kidogo cha (1) mara baada ya kuchapishwa itapelekwa bungeni kwaajili ya kudhibitishwa na Bunge na kanuni yoyote isiyothibitishwa itachukuliwa kuwa ni batili kutoka siku ilipokataliwa, bila ya kuathiri kitu chochote kilichofanyika kabla kulingana na mamlaka ya kanuni hizo.

SEHEMU YA IX
MABADILIYO YANAYOANDAMANA

Mabadiliko katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 Na.9 ya 1985

49.Kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 kimebalishwa katika kifungu kidogo cha (5) kwa kuondoa nukta mkato iliyopo kwenye kifungu (iii) cha aya (a) na kuweka nukta na kuongeza mara baada yake kipengele kifuatacho:

"(iv) Ugaidi dhidi ya Sheria ya Ugaidi, 2002."

Mabadiliko katika Sheria ya Usalama wa Taifa, 1970 Na. 3 ya 1970

50. Kifungu cha 10 cha Sheria ya Usalama wa Taifa, 1970 kinabalishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu hicho kifuatacho;

"Makosa yanayohusiana na ugaidi"

"10A. Mtu ambaye atatenda kosa dhidi ya vifungu vya 4, 5, 6, 7, 8, 9 au 10 katika mazingira ambayo inaweza kufikiriwa kuwa kosa lilitendeka ili kuendeleza au kuunga mkono kitendo cha kigaidi kinyume na Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002 atashughulikiwa chini ya Sheria hiyo"

Mabadiliko katika Sheria ya Upelekwaji, 1965 Na. 15 ya 1965

51. Kifungu cha 17 cha Sheria ya Upelekwaji, 1965 kinabadilishwa na kuongezwakifungu kidogo kifuatacho-

"(5) Vifungu vidogo vya (1) na (2) havitatumika kwa mtu anayetuhumiwa kwa ugaidi chini ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002"

Mabadiliko katika Sheria ya Mapato ya Makosa ya Jinai, 1991 Na. 25 ya 1991

52. Kifungu cha 6 cha Sheria ya Mapato yatokanayo na Makosa ya Jinai, 1991 kinabadilishwa-

(a) Kwa kuweka baada ya aya (b) kipengele kifuatacho-

"(c) kosa lolote dhidi ya Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002;"

(b) Kwa kubadilisha aya (c) kuwa aya (d).

Mabadiliko katika Sheria ya Uhamiaji,1995 Na. 7 ya 1995

53. Sheria ya Uhamiaji,1995 inabadilika-

(a) Katika kifungu cha 8 kwa kuondoa kifungu kidogo cha (1) na kuweka badala yake, kifuatacho:

"(1) Afisa uhamiaji anaweza bila hati kumkamata mtu yeyote ambaye anamshuku kuwa ni mhamiaji aliyekataliwa, gaidi au anajishughulisha na ugaidi wa kimataifa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya mwaka 2002 au amekwenda au anataka kwenda kinyume na kifungu chochote cha sheria hii".

(b) Katika kifungu cha 10,kwa kuweka nukta mkato badala ya nukta ambayo inaonekana katika aya (j) na kuongeza aya ifuatayo:

"(k) mtu ambaye ametenda kitendo cha kigaidi au ugaidi wa kimataifa."

Mabadiliko katika Sheria ya Ushahidi, 1967. Na. 6 ya 1967

54. Sheria ya Ushahidi, 1967 inabadilishwa katika kifungu cha 89-

(i) Kwa kukitaja kifungu hicho kuwa ni kifungu kidogo cha (1);

(ii) Kwa kuweka kifuatacho:

"(2) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) na sheria nyingine yoyote, katika mashitaka ya jinai ambayo yanahusu kosa la ugaidi au ugaidi wa kimataifa, swali likiibuka kuhusu kitu chochote kuwa katika hali iliyoelezewa katika nyaraka, nyaraka hiyo itapokelewa kama ushaidi bila ya kudhibitisha saini au mamlaka ya mtu aliesaini na ikiwa kutakuwa hakuna ushahidi wa kupinga, utakuwa ni uthibitisho wa maelezo yaliyoko ndani yake."

Imepitishwa na Bunge Tarehe 5/11/2002

Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

_____